

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA SEKOU - TOURE INATANGAZA NAFASI ZA AJIRA YA MKATABA KATIKA KADA ZIFUATAZO:-

1. Mhudumu wa chumba cha Maiti – Nafasi (4)

A. Sifa za Mwombaji za kuingilia moja kwa moja

- Elimu ya kidato cha nne na kuendelea
- Mafunzo ya afya au stahhada ndogo (certificate) inayohusiana na huduma za afya au uhudumu wa maiti.
- Uwezo wa kufanya kazi katika mazingira yenye changamoto.
- Nidhamu, uaminifu na kuheshimu Siri za kazi.
- Afya njema ya mwili na akili.
- Uwezo wa kufuata taratibu na maelekezo kwa umakini.
- Ujuzi wa msingi wa usafi na kinga dhidi ya maambukizi.

B. Majukumu ya Mhudumu wa chumba cha Maiti

- Kupokea na kuhifadhi miili ya marehemu kwa utaratibu unaofaa.
- Kusafisha na kuandaa miili kabla ya kuhifadhiwa au kukabidhiwa kwa ndugu.
- Kuweka kumbukumbu sahihi za miili (majina, tarehe n.k).
- Kuhakikisha usafi wa chumba cha maiti na vifaa vyake.
- Kufuata taratibu za usalama na kinga dhidi ya maambukizi.
- Kusaidia kaika utoaji wa miili kwa ndugu au taasisi husika.
- Kutunza vifaa vya kazi kama friji za kuhifadhi miili.

2. Afisa Tehama Msaidizi – Nafasi (2)

A. Sifa za mwombaji za kuingilia moja kwa moja

- i. Mhitimu wa kidato cha nne au cha sita , Stashahada ya Kompyuta katika moja ya fani zifuatazo; Sayansi ya Kompyuta, Teknolojia ya Habari na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Menejimenti ya Mifumo ya Habari au mafunzo mengine yanayohusiana na fani hii.

B. Majukumu ya Afisa Tehama Msaidizi

- i. Kuweka kumbukumbu na taratibu zote za kufanyia kazi.
- ii. Kutekeleza chati za mtiririko wa mifumo ya nyendo za taarifa na uhibititi.
- iii. Kuandika program za Kompyuta (Implement software systems (Write and document code).
- iv. Kufanya majaribio ya sehemu timilifu za programu za Kompyuta (Perform unit systems (module testing).
- v. Kufanya majaribio ya usanidi wa mifumo ya TEHAMA (Perform testing of system configurations).
- vi. Kufanya majaribio ya program za Kompyuta kulingana na mahitaji ya watumiaji (Conducting user acceptance test) na kusimamia mifumo yote inayotumika ndani ya hospitali.
- vii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazoendana na sifa na fani yake.

MAMBO YA KUZINGATIA KWA MUOMBAJI

1. Mwombaji wa kujitolea awe raia wa Tanzania mwenye *umri kuanzia miaka 18* na *usiozidi miaka 35* na awe hajawahi kuajiriwa katika Taasisi yoyote ya Umma.
2. Awe na cheti cha ufaulu cha kidato cha nne au sita.
3. Awe na cheti cha diploma ya taaluma husika.
4. Ambatisha wasifu (CV) yenye anuani na namba ya simu.
5. Awe na picha mbili za passport size za rangi.
6. Awe na nakala ya kitambulisho cha Nida.
7. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (NACTE na NECTA).
8. Barua ya uthibitisho/matokeo ya mtihani (Testimonial provisional/statements of results) Havitapokelewa.
9. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi, wahasika watachukuliwa hatua za kisheria.

Mwombaji atakayepata nafasi ya ajira ya mkataba atalipwa kiasi cha Tshs. 250,000/= kama muongozo wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora uliotolewa tarehe 24 Desemba, 2025 wenye Kumb. Na. HA. 151/200/01/12 Ulivyoelekeza.

- Barua zote za maombi zitumwe kwa:-

**Mganga Mfawidhi,
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mwanza,
S.L.P 132,
MWANZA.**

barua@sekoutourerrh.go.tz

Mwisho wa kupokea, Maombi ni Tarehe **07/05/2026** saa tisa na nusu Mchana.

Imeandaliwa na;

Beta
Dkt. Bahati P. Msaki
MGANGA MFAWIDHI (H)
MWANZA
24 Aprili, 2026

